# UADILIFU WA KWELI NA AMANI

*Hotuba ya Kufungia Mkutano wa Mwaka wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Uingereza 2015*

*na*

**Hadhrat Mirza Masroor Ahmad**

*Imamu na Kiongozi Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Duniani, Khalifa wa Tano wa Masihi Mau'udi*[as]
(*Allah Awe Msaidizi wake*)

JUMUIYA YA WAISLAMU WAAHMADIYYA
TANZANIA

# Uadilifu wa Kweli na Amani

*Tafsiri ya Kiswahili ya Hotuba ya Kufungia Mkutano wa Mwaka wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Uingereza tarehe 23 Agosti 2015 uliotolewa na Hadhrat Mirza Masroor Ahmad[aba], Khalifa wa Tano wa Masihi Mau'udi[as], na Kiongozi Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya Duniani.*

Chapa ya Kwanza: 2016
© Islam International Publications Ltd.

Kwa maelezo zaidi:

Tanzania:
Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya, Tanzania
Mtaa wa Bibi Titi Mohamed S.L.P. 376, Dare es Salam.
Simu: +255222110473 Fax: +255222121744
Kenya:
E.A. Ahmadiyya Muslim Mission
P.O. Box 40554 Nairobi, Kenya. Simu: +255222111031

Kimechapwa na: Ahmadiyya Printing Press
Dar es Salam, Tanzania
Simu: +255222111031

ISBN: 978-1-84880-546-0

# MAELEZO YA MWENEZI

Hadhrat Mirza Masroor Ahmad, Khalifatul Masihi wa tano[aba] alitoa hotuba ya kufungia Mkutano wa mwaka wa Uingereza tarehe 23 Agosti 2015 huko Hadikatul Mahdi, Alieleza umuhimu wa amani duniani na majukumu ya Waahmadiyya.

Mikononi mwenu ndiyo tafsiri ya hotuba hiyo. Sheikh Muzaffar Ahmad Durrani, Amiri na Mbashiri Mkuu wa zamani wa Tanzania akaitafsiri kwa lugha ya Kiswahili. Kisha nikaidurusu kwa makini kwa kuilinganisha na matini ya Kiurdu.

Sheikh Ansar Hussain na Seyid Tanwir Mujtaba nao wakasaidia kwa njia mbalimbali ili kukamilisha kazi hii. Mungu Awape wote hao malipo bora hapa na huko akhera.

Jamil R. Rafiq
Wakilut Tasnif, Tahrike Jadid
Rabwah, Pakistan.

10 Machi 2016

بِسۡمِ اللّٰهِ الرَّحۡمٰنِ الرَّحِیۡمِ

# HOTUBA YA KUFUNGIA

MKUTANO WA MWAKA WA UINGEREZA

23.08.2015

Baada ya kusoma shahada, audhu, Bismillahi na Suratul-Faatiha Khalifa Mtukufu Mungu Amsaidie alisema:

اِنَّ اللّٰہَ یَاۡمُرُ بِالۡعَدۡلِ وَ الۡاِحۡسَانِ وَ اِیۡتَآیِٔ ذِی الۡقُرۡبٰی وَ یَنۡہٰی عَنِ الۡفَحۡشَآءِ وَ الۡمُنۡکَرِ وَ الۡبَغۡیِ ۚ یَعِظُکُمۡ لَعَلَّکُمۡ تَذَکَّرُوۡنَ ○ [1]

Kwa hakika Allah Anaamuru uadilifu na hisani na kuwapa (watu kama uwapavyo) ndugu; na Anakataza upujufu, na uovu, na uasi. Anawanasihini ili mpate kufahamu.

Siku hizi machafuko yanayoenea duniani kote pote yamemfadhaisha kila mtu anayependa amani. Kila mtu anayehurumia ubinadamu anahangaika na kufadhaika kwamba inafanyika nini duniani! Kusema wanasema wasemao na inaandikwa pia mengi juu ya jambo hili kwamba machafuko haya yamezuka kwa nguvu zaidi

[1] An-Nahl, 16:91

katika ulimwengu wa Kiislamu, au sababu yake ni Waislamu, na kisha kwa sababu hii yaamuliwa kwamba dini kwa jumla na Islam hususan ndiyo chanzo cha machafuko, Mungu Apishe mbali. Mpaka sasa ulimwengu wa Kimagharibi ulikuwa ukifikiria kwamba machafuko hayo yote yataishia mpaka kwenye nchi za Kiislamu na nchi ambazo hazikuendelea, na hilo ndilo tatizo lao; nasi yaani tulioendelea tutadumu kuwasaidia kwa kutatua tatizo hilo na kujaribu kuimarisha pia uadilifu. Ni jambo lingine hili kwamba kwa kisingizio cha kusaidia au kuimarisha uadilifu, lengo moja pia lilikuwa kuthibitisha ubora wao na kunufaika pia na maliasili za nchi hizo. Lakini hiyo ilikuwa ni kosa la mataifa makubwa au la wapinga dini ambalo wakati umelihakikisha sasa kwamba hili halikubaki tu kuwa tatizo la nchi za Kiislamu. Mwelekeo wa siasa kali na ugaidi haukomi hadi nchi za Kiislamu, bali ukivuka utazikera nchi za magharibi na nchi zilizoendelea na utaziletea matokao yenye kutisha.

Naendelea kuwaelekeza hao tangu miaka michache iliyopita kwamba dunia iko katika hali ya machafuko, tunaidhani hali hii kuwa katika sehemu maalum tu; hiyo ni kosa letu. Wengi walikuwa wanakubaliana na maneno yangu kihulka tu lakini baadaye walikuwa wakisema kwamba dunia na hususan nchi zilizoendelea hazitakabili

hali za kutisha kiasi anachoeleza au inachoelezwa. Lakini leo viongozi hao hao na wachunguzi wa hali ya dunia wameanza kusema kwamba hali hii ya machafuko iliyopo duniani, kwayo sasa nchi zilizoendelea pia hazitasalimika, na hali hiyo yenye kutisha inakaribia kutumeza pia. Kauli ya Waziri Mkuu wa Uingereza pia inadhihirisha hatari hiyo. Waziri wa mambo ya nje wa Australia naye amesema hivyo hivyo. Mkuu wa zamani wa jeshi wa Uingereza pia amesema maneno kama hayo. Magazeti kadha pia yameanza kuandika. Ilmuradi, huu ni ukweli kwamba dunia imezungukwa na dhuluma na machafuko. Walioendelea au walioelimika kidunia wanadhani kwamba dini imesababisha hiyo na imefikia kilele chake kwa sababu ya kundi moja la kidini la Waislamu; lakini kwa kweli hiyo ni kwa sababu ya kutoelewa dini. Dunia inadhani kwamba kwa kumaliza machafuko hayo tunahitaji kuachana na dini. Jambo hili linatangazwa sana. Magazeti nayo yanaeneza kwamba dini inamfanya mtu kuwa ama jahili na mzembe au mwenye siasa kali. Na kama mkitaka kupata maendeleo, basi maendeleo yaweza kupatikana kwa kutengana na dini. Hao watu wanadhani kwamba maeandeleo yapatikana kwa kukaa tu mbali na Mwenyezi Mungu. Kwa kueneza nadharia hii potofu, idadi ya wakana Mwenyezi Mungu inaendelea kuongezeka siku hadi siku, ilihali ukweli wenyewe ni

kwamba kwa kumsahau Mwenyezi Mungu dunia imetumbukia katika machafuko. Machafuko haya ni kwa sababu ya kutumia vibaya mafundisho ya Mwenyezi Mungu, na kwa kutumia jina la Mwenyezi Mungu kwa kujipatia manufaa yao, au kwa kukanusha kuwepo kwa Mwenyezi Mungu, bali ni kwa kuruka mipaka yote katika kumfanyia Mwenyezi Mungu dhihaka.

Ilmuradi sababu ya msingi ya hali ya machafuko duniani ni kujinyakulia manufaa ya binafsi kwa jina la Mwenyezi Mungu na kutokwa na hofu Yake ya kweli mioyoni, au kwa kukanusha kuwepo kwa Mwenyezi Mungu kutanguliza kanuni na nadharia zao za kidunia juu ya kila kitu. Mtu akiwa kiumbe cha Mwenyezi Mungu anajiona bora na anazifikiria kanuni za Mwenyezi Mungu na nidhamu yake ya uadilifu kuwa duni kuliko kanuni na nidhamu ya uadilifu alizounda yeye, na anauliza kwa nini hatuwezi kuyafanya mafundisho ya dini sawa na haja ya zama yafuate mila za kidunia, matamanio ya kidunia na kanuni za kidunia. Mwulizaji mmoja, msomi, profesa wa chuo kikuu aliniuliza hayo mimi pia. Lakini, kumbukeni kwamba kama mafundisho ya dini yamekwisha haribika na kama viwango na kanuni za asili za kibinadamu zaweza kuvishinda viwangu na kanuni za asili za Mungu, hapo swala hilo laweza kuzaka. Lakini tunakiamini kitabu

ambacho kimehifadhiwa tangu miaka elfu moja na mia nne na ambacho mafundisho yake ni bora kabisa kwa kila jiha na ni utaratibu kamili wa maisha kwa binadamu wa zama zote ambacho kimeteremshwa na Mungu, Mola wa walimwengu na Mjuzi wa siri na dhahiri; hakina haja kiwe chini ya kanuni ya binadamu. Dini inakuja kuwafanya wanadamu waifuate, haiji kwa kufuata dunia au matamanio ya watu hao. Na leo Islam ni ile dini na Kurani Tukufu ni kile kitabu kinachowaongoza watu wa zama zote, sharti mtu awe na uwezo wa kuielewa. Leo haki zinanyang'anywa duniani, hiyo haiifanyi dini, bali huifanya kanuni za kidunia au wadanganyifu kwa jina la dini. Leo dhuluma zinazofanyika katika sura ya vita na mapigano, hizo hazifanywi na dini, bali dunia kwa masilahi yake inafanya. Leo khulka mbovu zinazoonekana kwa jina la uhuru na upujufu sio sehemu ya mafundisho ya dini, bali ni kwa sababu ya ubovu wa kanuni za binadamu zilizovuruga amri za Mwenyezi Mungu. Kuonyesha nguvu na ubora sio mafundisho ya Mwenyezi Mungu, bali ni uzushi wa binadamu kwamba mtu ajione mbora kuliko kila kitu.

Basi, mambo hayo tunayoyaona siku hizi duniani, hayo ni kwa sababu ya kujidhania kuwa mwenye akili yote na kwa

kukosa nuru ya wahyi. Na hiyo ni hali ambayo imetajwa katika Kurani Tukufu. Akasma:

ظَهَرَ الْفَسَادُ فِى الْبَرِّ وَالْبَحْرِ بِمَا كَسَبَتْ اَيْدِى النَّاسِ لِيُذِيْقَهُمْ
بَعْضَ الَّذِىْ عَمِلُوْا لَعَلَّهُمْ يَرْجِعُوْنَ ○[2]

Maovu waliyotenda watu yamesababisha ufisadi kutapakaa bara na bahari ili Awaonjeshe matokeo ya baadhi ya amali zao, huenda wakarejea.

Basi, hayo ndiyo kwa sababu ya machafuko yaliyoanzishwa na mwanadamu, ambayo hayuko nje yake tajiri wala masikini, wala watu wa dini yaani wa dini kwa jina tu wala watu walioachana na dini. Katika hali kama hizo ni dhahiri kwamba mtu atashikwa na Mwenyezi Mungu na atapata adhabu ambayo ni kwa sababu ya kuwa mbali na Mwumba na ndiyo matokeo yake hayo. Tutakapokuwa mbali na Mwenyezi Mungu, basi ni dhahiri kwamba kwenda mbali na Mwumba na Mmiliki wa dunia hii, matokeo yayo hayo yalipaswa kutokea na yanatokea na Mwenyezi Mungu Anaadhibu pia kiasi fulani, na adhabu itakayotolewa katika akhera ya amali hizo, Mwenyezi Mungu Anaijua na Anajua vizuri. Lakini Mwenyezi Mungu hafurahi kuwaadhibu watumishi wake. Mwenyezi Mungu ndiye ambaye Anafurahia kuja kwa

[2] Ar-Ruum, 30:42

mja wake kwenye njia sahihi na kuwaona wale wanaotengana na machafuko, zaidi kuliko yule mama anayefurahi kupata mtoto wake aliyepotea katika hali za kutisha. Wakati anapoendelea kumtafuta mtoto wake kama majununi na anahangaika hapa na pale baina ya hali ya tamaa na kukata tamaa kwa kutojua kwamba mtoto wake yu hai au la, kisha ghafla anampata na anamkumbatia. Kiasi anachofurahi huyo mama, Mwenyezi Mungu Anawapenda waja wake zaidi yake. Mtu anapomwelekea Mwenyezi Mungu, Yeye Anapata furaha zaidi kuliko hiyo yake. Na Mwenyezi Mungu kwa sababu ya mapenzi yake Anawatuma mitume wake kwa kurekebisha dunia na kwa kuwaonyesha njia sahihi ili dunia isalimike na maangamio na ijikinge pia katika kuadhibiwa kwa sababu ya maovu na machafuko. Mwenyezi Mungu Anataka kwamba Awalinde watu wasianguke motoni; na sio tu kuwalinda kuanguka motoni tu bali Awaneemeshe. Kuhusu hali hii na zama hizi Sayyidna Ahmad a.s. anasema: Wakati huu watu wanataka maji ya kiroho. Ardhi imeshakufa kabisa. Zama hizi zimekuwa ظَهَرَ الْفَسَادُ فِي الْبَرِّ وَ الْبَحْرِ[3] Mapori na bahari zimeharibika. Pori lamaanisha washirikina na maana ya bahari ni watu wa Kitabu. Yaweza pia kumaanisha jahili

[3] Ar-Ruum, 30:42

na mtaalamu. Ilmuradi, katika kila tabaka la wanadamu machafuko yameenea. Ukitazama kwa jiha yoyote na namna yoyote, hali ya dunia imeshabadilika; haukubaki wema, wala hata athari zake hazionekani. Kila mdogo na mkubwa ameshashikwa na unyonge wa khulka na amali. Ucha Mungu na maarifa ya Mungu vimetoweka. Kwa hiyo, wakati huu kuna haja ya maji ya kimbingu na wa nuru ya unabii kuteremka na kuing'arisha mioyo yenye bidii. Mshukuruni Mwenyezi Mungu ambaye kwa fadhili yake Ameteremsha wakati huu nuru hii, lakini ni wachache wanaofaidika na nuru hiyo:[4]

Basi, Mwenyezi Mungu Anatimiza suna yake kwa kasalimisha ubinadamu, na Anatuma Mitume wake kwa kuongoza barabara dunia na kuwaonyesha njia za kujikinga na machafuko. Katika zama hizi pia Amemtuma Hadhrat Masihi Mau'udi a.s. Hali za dunia zinatuonyesha kwamba hali ya Waislamu imeshaharibika jinsi alivyoeleza mhutubu mmoja mgeni kuhusu nchi moja, na ndivyo ilivyo hali ya dini zingine na ya wale wasiokuwa na dini. Kile inachokimbilia dunia si maji bali ni sarabi. Maji hasa na nuru ndiyo Aliyoteremsha Mwenyezi Mungu. Badala ya Waislamu na watu wengine kushukuru na kupata mwanga katika nuru hii na kunywa

[4] Malfudhat, J. 4, uk. 444

maji kutoka katika chemchemi hii, wanaendelea kuzama katika giza na wanakunywa maji ya mabwaba machafu. Kwa bahati mbaya Waislamu pia hawamthamini mtumishi mkweli wa Mtume Mtukufu[saw]. Wanawafuata maulamaa waovu wakiyadhania maji machafu kuwa maji safi. Wafuasi wa dini zingine pia badala ya kutambua ukweli wanaleta vipingamizi, matokeo yake ni kwamba dunia inaendelea kuchoka na dini, inakana uwepo wa Mwenyezi Mungu. Ingawa Waislamu wengi wako imara juu ya dini yao kimadai au kiitikadi, lakini masheikh wakiwapumbaza wamewaharibia kabisa hali zao kielimu na kimatendo. Na sio kwamba nawakosoa tu, ukweli huu haukufichika kwa yeyote. Katika nchi za Waislamu machafuko, ugaidi na mauaji kwa jina la dini, Mungu na Mtume yaliyopo yapo mbele ya dunia. Dhuluma za serekali juu ya raia, na uasi wa raia na dhuluma ni thibitisho la jambo hilo. Kisha watu wa kawaida wanapowaendea maulamaa kwa kupata mwongozo, hawaoni hapo chochote isipokuwa ubinafsi. Kauli ya Mtume Mtukufu[saw] inatimia barabara kwamba hakitapatikana chochote kutoka kwa maulamaa isipokuwa fitina. Kauli zao na amali zao zitapingana, haitaweza kupatikana chochote kutoka kwao isipokuwa mambo ya ujahili na fatuwa. Basi mambo na matendo ya

maulamaa wa siku hizi pia ni thibitisho la ukweli wa Mtume Mtukufu[saw][5]

Tena Waislamu kwa jumla wameanguka vibaya kihulka, na kurudi nyuma kidini kunaonekana wazi. Maulamaa wakiwa majahili na wakitoa fatuwa kuangalia manufaa yao, basi ni dhahiri hali ya dini ya Waislamu wa kawaida itakuwaje. Maulamaa hao wamegeuza mafundisho ya Islam kwa manufaa yao kiasi hiki kwamba imekuwa halali kunyang'anya haki za wengine. Fatuwa kama hizi zimekuwa ni kawaida sasa katika Pakistan kwamba Waahmadiyya kwa kuwa wako nje ya Islam — ingawa wanatamka لا اله الا الله محمد رسول الله au waendelee kutamka — lakini kwa vile wapo nje ya Islam, kwa hiyo inajuzu kuteka na kunyan'ganya mali yao. Wao wenyewe pia wamegawanyika katika makundi mbalimbali na mioto ya chuki inawaka. Mwenyezi Mungu Anasema: رُحَمَآءُ بَيْنَهُمْ [6] lakini badala ya upendo huo na udugu, uadui mkali unaendelea kuzidi baina yao. Basi hii ni dalili ya jambo hili kwamba hali hii ya machafuko ipo ndani ya Waislamu pia, na rehema ya Mwenyezi Mungu ilihitaji kwamba wakati kama huu Angemtuma mtume wake yeyote, na Mwenyezi Mungu Akamtuma sawa na suna na

---

[5] Al-Jami' lishua'bil-Iman Lil-Baihaqi Juzuu 3, uk. 317-318, Hadith Na. 1763, Maktabah Ar-Rushd 2004.

[6]Al-Fat'h, 48:30

ahadi yake. Lakini kama nilivyosema, maulamaa wakiwaongoza Waislamu vibaya, wakawazidisha katika upinzani wake badala ya kumwamini yeye. Na badala ya kusema kwa kuitikia sauti ya ajaye wakifuata kauli ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake na kujaribu kuwa umati mmoja, wakampinga na kuangukia fitina, ufisadi na mauaji baina yao, na wanawatilia wengine athari yao mbaya. Ndiyo sababu wapinzani wasiokuwa Waislamu wanatumia vibaya udhaifu huu wa Waislamu. Wanaipinga Islam, wanaishambulia Islam, wanaitaja Islam kama dini ya fitina, ufisadi na siasa kali, na wanajaribu kuthibitisha kwamba wasiokuwa Waislamu na walioachana na dini kuwa waimarishao amani duniani na waenezao suluhu na amani. Lakini hawayasemi hayo yote kinaganaga, bali wanafanya hila zao kwa ujanja sana. Upande mmoja wanadai kuwa na huruma kwa Waislamu na mahusiano nao ya amani na usalama, wanajitolea kwa huduma ya kukomesha fitina na machafuko katika nchi za Kiislamu, upande mmoja wanasema kwamba Islam si dini mbaya, Waislamu si wabaya, Islam haifundishi ugaidi na dhuluma, na twapaswa kujaribu kwa pamoja kumaliza machafuko ya dunia ambamo machafuko mengi zaidi ndiyo ya nchi za Waislamu. Lakini upande wa pili wanasema hii pia kwamba Islam, ugaidi na siasa kali vina mahusiano. Wanasema hii pia kwamba siasa kali hiyo ni

kwa sababu ya mafundisho ya Islam. Wakisema mambo mawili wakati mmoja — au kumfanya kiongozi mmoja aseme jambo moja na mwingine jambo jingine — wanataka kuwafurahisha wapinzani wa Waislamu pia na wanataka kuwafurahisha Waislamu vilevile. Twawaambia hao kwamba mafundisho ya Islam ndiyo mafundisho ya kuweka msingi wa amani, usalama na suluhu — mafundisho ambayo hakuna mafundisho mengine yanayoweza kuyakabili. Wasemao dhidi ya Waislamu wanapaswa kuzingatia jambo hili kwamba kwa kusema hayo wanawasaidia makundi ya Waislamu wa jina wenye siasa kali. Kwa kusema hayo wanawachokoza Waislamu wasioelimika, wasio na utulivu kwa sababu ya hali zilivyo. Juhudi za kuimarisha amani hazitafua dafu kwa kuilaumu dini, bali wekeni dini kando, kisha tieni bidii dhidi ya dhuluma, ndipo kazi hii itafanyika. Kama mkitekeleza wajibu wenu kwa kufanya kazi dhidi ya dhuluma, hapo mtapata ufaulu. Basi watu hao wahusikao na mataifa makubwa ambao ni viongozi wa serekali, hao wanahitaji kuweka msingi wa sera yao juu ya uadilifu. Hakuna shaka kwamba watu wa dunia hawana mtazamo wa kidini, kwa hiyo wanaona kwa mtazamo wa kidunia, na kidhahiri juhudi za kuleta amani zinakuwa njia za uchafuzi. Kwa hiyo, mataifa makubwa yasijivunie nguvu zao. Kama shabaha ni kuimarisha amani duniani, basi haya mataifa

makubwa pia yalazimika kubadilisha mienendo yao; la sivyo kumbukeni kwamba dunia nzima itashikwa na machafuko na vita kwa nguvu zaidi. Kadhalika, Waislamu pia wanalazimika kusikiliza sauti ya Mwenyezi Mungu, na wanapaswa kuchunguza kaulimbiu mbovu za maulamaa, viongozi na vyama vya jina kwa vigezo vya mafundisho ya Mwenyezi Mungu sio kwa vigezo vyao. Angalieni kwamba mafundisho mema ya Islam ni nini? Angalieni kwamba Mwenyezi Mungu Anawatakieni nini? Mwenyezi Mungu Anataka kwamba mwelekee kwake aliyetumwa Naye. Na itakapofanyika hayo, basi hitilafu za wenyewe kwa wenyewe zikiisha, upendo, mapenzi na uadilifu vitaimarika. Umma wa Kiislamu utakuwa umma mmoja na matokeo yatakuwa kwamba wale walionaswa katika utumwa wa nchi zisizokuwa za Kiislamu watapata wokovu na uhuru. Daima tunapaswa kukumbuka kwamba mafundisho na nidhamu ya kimagharibi au ya kidunia sio dhamini za amani na usalama wala haviwezi. Dhamini ya amani na usalama wa dunia ni mafundisho ya Kiislamu ambayo hayakutolewa na dini yoyote kabla ya Islam wala hayapo katika falsafa, nadharia na nidhamu ya zama hizi. Ni mafundisho mazuri ya Islam yaliyo dhamana ya amani, usalama na mapenzi.

Basi, leo badala ya mataifa yasiyokuwa ya Kiislamu kutuonyesha njia za amani na usalama, tunapaswa

kuyaonyesha hayo njia za amani ya kweli na uadilifu katika mwanga wa mafundisho ya Kiislamu, na mafundisho hayo yanang'ara katika aya ile ndogo niliyoisoma sasa hivi. Basi, kila Mwislamu anapaswa atafakari jambo hili. Badala ya kujitetea tu, kuna haja ya kuweka mafundisho hayo yang'arayo mbele ya dunia kwa changamoto. Basi, leo katika mwanga wake pia nitaeleza kuhusu mafundisho yaliyomshukia Mtume Mtukufu s.a.w., ambayo makhalifa zake ma-Rashidina na baadhi ya wakuu wa serekali wasio na ubinafsi, wenye kuhurumia umati waliyafanya yatekelezwe na kuimarishwa katika zama zao, nao wakaimarisha jamii nzuri. Sikanushi pia ukweli huu kwamba mafundisho hayo mazuri yalifunikwa na mienendo ya ubinafsi ya serekali nyingi za baadaye, na manufaa ya binafsi ya watawala Waislamu na maulamaa. Lakini kama nilivyosema, Mwenyezi mungu anatuma mitume wake kwa kuwaongoza wanadamu katika kila zama za machafuko, Yeye ndiye Aliyemtuma Hadhrat Masihi Mau'udi a.s. pia aliyetufahamisha vizuri uzuri wa mafundisho hayo mazuri. Yeye alitangaza kwamba kuna makusudio mawili ya ujaji wangu. Mosi, kumwunganisha mtu na Mwenyezi Mungu na kuelekeza kwenye utoaji wa haki ya Mwenyezi Mungu, na ya pili ni

kuwafanya watu watoe haki za wanadamu wengine.[7] Basi, Islam inatuelekeza kutoa haki hizo mbili, nasi tunapaswa kuliona hilo katika mwanga wa mafundisho ya Kurani Tukufu. Na kama nilivyosema, twaona sawa na aya hiyo namna vinavyoimarika viwango vya haki hizo, na namna iwezavyo kuimarika uadilifu, upendo na udugu, jinsi Mtume Mtukufu s.a.w. alivyotuonyesha mfano wake mwema kwa kitendo. Katika zama hizi pia twaona namna mjumbe wa Mwenyezi Mungu alivyotuongoza kutokana na aya hiyo kutoa haki za aina zote hizo mbili.

Hadhrat Masihi Mau'udi a.s. anasema: Amri kubwa za Kurani Tukufu ni mbili tu. Ya kwanza, umoja wa Mwenyezi Mungu na upendo Wake na utii Wake. Pili, huruma ya ndugu na wanadumu wote. Na imezigawa amri hizo katika madaraja matatu. Anasema akitaja aya takatifu hii إِنَّ اللّٰهَ يَأْمُرُ بِالْعَدْلِ وَالْإِحْسَانِ وَإِيتَآئِ ذِى الْقُرْبٰى kwamba maana ya kwanza ya aya hii ni kwamba kwa kumtii Mwumba wenu mfuate njia ya uadilifu; msiwe wadhalimu. Basi, kama vile kwa kweli hakuna apasaye kuabudiwa isipokuwa Yeye, hakuna apasaye kupendwa, hakuna apasaye kutegemewa, kwani kwa sababu ya sifa zake za uumbaji, na ulezi kila haki ni yake tu (Yeye ndiye Aliyetuumba, Ndiye Anayetuhuisha na kudumisha,

---

[7] Malfudhat, J. 3, uk. 95-96.

Ndiye Anayetupatia mahitaji ya malezi yetu, hivyo, hii ndiyo haki yake.), hivyo nanyi pia msimshirikishe na yeyote katika ibada yake na mapenzi yake na katika uungu wake. Kama mkiishafanya kiasi hicho, basi huo ndio uadilifu ambao kuujali kulikuwa ni faradhi yenu. Kisha mkitaka kuendelea mbele zaidi, basi kuna daraja ya hisani, na hiyo ndiyo kwamba mwamini adhama zake na mnyenyekee katika ibada zake na mjisahau katika mapenzi yake kiasi hiki kana kwamba mmeshaona adhama yake na jalali yake na jamali yake ya milele. Baada yake ipo daraja ya *Itai dhil Kurbaa.* Na hiyo ndiyo kwamba ibada yenu na mapenzi yenu na utii wenu utengana na urasmi na kujifanya visivyo, na mumkumbuke kwa moyo wote kama —kwa mfano — mnavyowakumbuka baba zenu, na muwe mwampenda kama mtoto anavyompenda mama yake mpendwa. Na maana ya pili ya aya hii inahusikana na huruma ya wanadamu, nayo ni kwamba wafanyieni uadilifu ndugu zenu na wanadamu wote na msing'ang'anie kuchukua zaidi ya haki zenu (zilizo haki zenu jaribuni kuzipata; msijaribu kuchukua zaidi yake), na simameni imara juu ya uadilifu. Na kama mkitaka kuendelea mbele zaidi ya daraja hii, basi kuna daraja ya hisani mbele yake, nayo ni hii kwamba badala ya ubaya wa ndugu yako umtendee wema, na badala ya udhia wake mpe raha, umsaidie kwa

ukarimu na hisani. Kisha baada yake kuna daraja ya *Itai dhil Kurbaa*, nayo ndiyo kwamba kiasi chochote utakachomtendea wema ndugu yako au kiasi chochote utakachowahurumia wanadamu, usiwe na nia ya kufanya hisani ya aina yoyote, bali wema huo utendeke kwako bila shabaha yoyote maalum. (Utende wema bila ya kunuia kufanya hisani. Akasema:) Wema utendeke kwako bila shabaha yoyote maalamu kama vile ndugu anavyomtendea ndugu yake, jamaa kwa jamaa yake na jamaa wa karibu kwa jamaa wa karibu, kwa jazba ya udugu. Basi huu ndio upeo wa maendeleo ya khulka kwamba katika kuwahurumia viumbe isiingilie kati shabaha yoyote ya nafsi au kusudio lolote au gharadhi yoyote, bali jazba ya udugu na uhusiano wa karibu wa kibinadamu upate kukua sana mno hata kwamba wema ule utendeke wenyewe kwa jazba ya asili bila kujikalifisha na pasipo kutamani kushukuriwa au kuombewa au kulipwa kwa namna yoyote.[8]

Basi maadamu wazo na utambuzi wa kutoa haki za aina zote mbili hauzaliki, madai ya mtu kuuimarisha uadilifu huwa madai matupu tu. Kanuni za kibinadamu haziendi mbele ya mipaka ya uadilifu, wala haziwezi, na wanadhani kwamba kwa kuimarisha uadilifu, hatua zote

[8] Izaala Auhaam, J. 3, uk. 550-552.

zimeshachukuliwa kuimarisha amani duniani; tumeshapata tuliyotakiwa kupata. Lakini hapa pia pana dhuluma. Kama yapo manufaa ya binafsi, basi masharti ya uadilifu hayatimizwi; na hii ipo katika nchi tajiri na pia katika nchi maskini. Kisha kama wakijibidiisha sana, wanajaribu kutenda hisani, lakini hisani hiyo sio katika wajibu wao. Na ndiyo sababu baada ya kufanya hisani anayesaidiwa anasimbuliwa pia, au tunaona duniani kwamba kama mtu akifikiriwa kupewa zaidi ya haki yake kwa jina la huruma, hapo pia baadhi ya masharti yanawekwa; na hilo twalishuhudia siku hizi sana katika mienendo na matendo ya serekali kubwa. Nchi maskini zinaposaidiwa, baadhi ya masharti yanawekwa; lakini sawa na mafundisho ya Islam msaada unaofuatwa na masimbulizi na udhia sio wema. Mungu Anasema:

لَا تُبْطِلُوْا صَدَقٰتِكُمْ[9]

Hadhrat Masihi Mau'udi a.s. ameieleza hivi kwamba enyi wafanyao hisani msiharibu sadaka zenu — zinazopaswa kutolewa kwa nia ya kweli — kwa kusimbulia na kuudhi.[10]

Basi, usipobaki moyoni ukweli na ikhlasi, sadaka na msaada vinavyotolewa kumsaidia maskini haviwi tena

[9] Al-Baqara, 2:265

[10] Ruhani Khaza'in J. 10, uk.354.

msaada na sadaka, na hapo haiwezi kubaki duniani fikara ya *itai dhil kurbaa*.[11] Hivyo, kama nilivyosema, katika kanuni ya dunia, kanuni yaweza kwenda mpaka uadilifu, na hiyo nayo kwa maneno tu matupu, kwani wakati wa kufanya uadilifu kwa udhuru mbalimbali uadilifu pia unapotezwa. Lakini Mwenyezi Mungu Anasema kwamba Mungu Anawaamuruni kuimarisha uadilifu, kufanya hisani na kutoa haki za jamaa wa karibu. Mnapaswa kuwa wenye kutimiza mahitajio ya uadilifu kitimilifu. Hisani yenu isifuatiliwe na udhia na usumbufu, na pia msiyaone mambo hayo mawili ya awali kuwa mwisho wenu, bali mzingatie pia muradi wa *Itai dhil kurbaa*, watendeeni wengine wema kwa huruma isiyo na ubinafsi. Uchukulieni uchungu wa wengine kuwa uchungu wenu, na hii ndiyo hali inayowafanyeni waumini.

Sasa angalieni shani ya amri iliyotolewa na Mwenyezi Mungu na kanuni iliyoundwa naye kwamba msipoimarisha pasipo ubinafsi viwango vya uadilifu, hisani na mapenzi hamwezi kuwa dhamana ya amani na usalama. Mafundisho hayo yanamfikisha mtu kwenye kilele cha utoaji wa haki za mtu mwingine. Kuhusu kuhurumia viumbe vya Mwenyezi Mungu na kuhusu kuimarisha amani na usalama, sio tu kanuni za dunia hata

[11] An-Nahl, 16:91

dini nyingine yoyote pia haiwezi kutoa mafundisho hayo, wala dini yoyote haikutoa mafundisho kama hayo. Kwa kutoa haki za binadamu na kwa kuimarisha amani na usalama, ni mafundisho ya Kiislamu tu yaliyopo palipo juu kabisa. Kama anayeitwa Mwislamu akitenda kinyume cha mafundisho hayo au serekali fulani ya Kiislamu au kundi fulani la Waislamu wa jina tu latenda kinyume cha mafundisho hayo au ladhihirisha siasa kali na dhuluma, hufanya dhidi ya mafundisho ya Kurani. Islam imewasisitizia waumini wake wa kila tabaka kufuata amri hii wakati wote. Kitendo kisichotakikana cha mtu kwa jina la Islam sio dalili ya jambo hili kwamba mafundisho ya Islam yanampa leseni au ruhusa ya kutenda kilicho ghalati. Wapinzani wa Islam wanaojifikiria kuwa wasimamizi wa uadilifu na amani wanapaswa watoe kauli zao wakifuata uadilifu. Viongozi na wanasiasa wa hapa wanaotoa maoni kwamba hatuwezi kukanusha jambo hili kwamba mafundisho ya Islam na ugaidi havihusikani, lazima upo uhusiano kiasi fulani. Huo ni ufinyu wa ujuzi wao, au wanayoeleza hao ndiyo kinyume cha adili. Hawaoni vitendo vyao kwamba wanavunjilia mbali uadilifu namna gani kwa jina la kuimarisha amani, wanafanya dhuluma namna gani sana. Sina haja ya kutoa maoni yangu juu yake, waandishi wao wenyewe wanafichua siri yao ya "kuimarisha" uadilifu na amani.

Mwandishi wa habari Bw. John Wight ameandika makala moja katika gazeti fulani juu ya “West’s Libyan Legacy”, ambamo amesema kwamba kati ya mifano ya mataifa ya Magharibi kuingilia kati mambo ya nchi zingine, hakuna mfano mbovu zaidi wenye kuangamiza kuliko ule wa kuhusu Libya. Nato iliingilia kati Libya, matokeo yake, nchi iliangamia. Kampeni ya Nato iliigawa nchi iliyokuwa inaendelea na kuirudisha nyuma kwenye mtindo wa kikabila ambako Daish imeshaimarika. Kumbukeni jambo hili, anaandika tena, kumbukeni jambo hili kwamba kabla Nato ilikuwa haijaingia katika Libya, kulikuwa hakuna huko vituo vya mafunzo ya ugaidi. Mataifa ya magharibi hayakumotishika kuleta mabadiliko ya kidemokrasia, bali yalitaka kufungua mlango wa ugunduzi wa mafuta na yalitaka kuimarisha mahusiano ya kiuchumi.[12] Huu ndio mfano kidogo wa dhuluma kwa jina la amani na uadilifu. Kadhalika waandishi wengi sana waliandika mengi kuhusu vita ya Iraki kwamba ilikuwa ni kosa, na pia kuhusu dhuluma nyinginezo. Angalieni mafundisho ya Islam wanayoyapinga, sawa nayo uadilifu ni wema mdogo kabisa. Uadilifu sio wema mkubwa sana. Islam inasema uadilifu ndio wema mdogo kabisa kabisa.

---

[12] John Wight, “Chaos & lawlessness”: The West’s Libyan legacy,” RT.com, published August 10, 2015,
https://www.rt.com/op-edge/312075-libya-chaos-war-west/

Hao wakipiga kelele za “uadilifu” wauita wema mkubwa. Haya, kama huo tu wakitekeleza, yaweza kusemwa kwamba hao ni watu wa dunia, kwao huo ndio wema mkubwa. Lakini pale palipo manufaa yao — kama nilivyosema hapo kabla pia — vigezo vyao vya uadilifu pia vinabadilika. Kuhusu hilo, Islam yaweka kigezo kizuri sana kwamba uadilifu uimarishwe namna gani, kigezo chenyewe kiwe kipi. Mungu Anasema:

يَٰٓأَيُّهَا ٱلَّذِينَ ءَامَنُوا۟ كُونُوا۟ قَوَّٰمِينَ لِلَّهِ شُهَدَآءَ بِٱلْقِسْطِ ۖ وَلَا يَجْرِمَنَّكُمْ شَنَـَٔانُ قَوْمٍ عَلَىٰٓ أَلَّا
تَعْدِلُوا۟ ۚ ٱعْدِلُوا۟ هُوَ أَقْرَبُ لِلتَّقْوَىٰ ۖ وَٱتَّقُوا۟ ٱللَّهَ ۚ إِنَّ ٱللَّهَ خَبِيرٌۢ بِمَا تَعْمَلُونَ[13]

Enyi mlioamini! Kuweni wasimamizi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu, mtoao shahada kwa adili. Na uadui wa watu usiwashawishini ya kwamba msifanye uadilifu. Shikeni adili, hiyo ni karibu sana na utawa, na Mcheni Mwenyezi Mugnu. Hakika Mwenyezi Mungu Anazo habari za yale mnayoyatenda.

Basi, hayo ndiyo mafundisho mazuri ya Islam. Katika uadui pia hakuna kujitafutia udhuru mbovu. *Kawwam* lamaanisha kutekeleza jambo fulani kwa njia sahihi na kwa uthabiti. Basi, amri ni kuuimarisha uadilifu, ni kuuimarisha kwelikweli, na ni kuuimarisha kwa uthabiti. Hiyo ndiyo anayoamrishwa Mwislamu. Na kumbukeni

---

[13] Al-Maaidah, 5:9

daima kwamba mwatakiwa kufanya kazi zenu mkizingatia amri za Mwenyezi Mungu. Mumini anatakiwa kutimiza mapasiko ya uadilifu kwa kuzingatia barabara amri za Mwenyezi Mungu. Mumini anapaswa kukumbuka daima na kuendelea kujitafutia kwamba Mwenyezi Mungu Anatuamru nini. Mtakapokuwa na hali hiyo, ndipo mtaitwa Waislamu wa kweli. Kuhusu uadilifu daima zingatieni amri hii ya Mwenyezi Mungu kwamba uadui wa watu fulani usiwapelekeni mbali na uadilifu. Sasa Mwenyezi Mungu Anapowasisitiza Waislamu kuwafanyia maadui uadilifu, basi na Anasisitiza kutenda wema mwingine pia. Sasa kama alivyoandika mwandishi huyo, vita ya Iraki au kumwondoa Kadhafi, sababu zake zilikuwa za kiuchumi tu na haikuwa zaidi yake, kujinyakulia utajiri wa mafuta pia ilikuwa shabaha. Mafundisho ya Kurani waliyopinga kwamba yafundisha ugaidi, Kurani inasema kwamba usitazame mali ya watu kwa tamaa. Niliposema jambo hilo huko Merekani mbele ya wanasiasa, mwanasiasa mmoja Mwamerika wa asili ya Kiafrika akaja kwangu na akasema jambo ulilosema kwamba msitazame mali ya watu kwa tamaa wala msijifaidishe na mali yao bila haki, hilo ni kweli tupu na sahihi, nasi tunalihitaji sana hapa.

Hii ni hali yao wenyewe; wanawezaje kuilaumu Islam hao watu! Sasa waandishi wao wameanza kuandika kama

nilivyomtaja mmoja wao. Ninayo makumbukumbu mengi walimoandika kwamba baadhi ya makundi ya ugaidi ya Waislamu ndiyo matokeo ya vita yetu ya Iraki na kwa sera za dhuluma katika nchi hizo. Katika vita kuu ya pili, mabomu waliyotupia miji miwili ya Japan na wakawaua ovyo raia wengi wasio na hatia, huo ulikuwa uadilifu gani? Ilikuwa ni huruma gani ya kibinadamu iliyodhihirika wakati ule? Au sasa imetokea nini kwamba swala hilo linaibuliwa tena. Hata leo watu hao wanaidhihirisha. Wanaweza hao kusema leo kwamba ni kosa lililotendeka wakati huo, halikupaswa kufanyika hivyo; lakini hata leo pia hawajutii kitendo chao hicho. Clifton Truman ambaye ni mjukuu wa Rais Truman, alisema katika mahojiano fulani kuhusu bomu kuwa lilikuwa ni kitu adhimu sana. Kuhusu babu yake alisema kwamba yeye alikomesha vita na akasalimisha watu wa nchi za pande zote mbili, na ndivyo babu yangu alivyoeleza sababu ya uamuzi wake. Alisema, sioni Marekani inapaswa kuiomba radhi kabisa Japan. Vilevile mwandishi mmoja aliandika katika Daily Telegraph la tarehe 9 Agosti kwamba mauaji ya watu kwa kutupia mabomu mijini Nagasaki na Hiroshima yalijuzu. Hiyo ndiyo hali yao, na hizo ndizo fikira zao! Vita yaendelea baina ya majeshi, lakini wanaouliwa ndio watoto, wazee na wanawake, wasio na hatia. Huu ndio uadilifu

wanaojitafutia udhuru kwamba kama isingekuwa hivi basi ingekuwa vile. Lakini kama kundi fulani la Waislamu linatenda kisichotakikana, huwa wanajaribu kulihusisha kwa mafundisho ya Kiislamu. Mafundisho ya Islam ndiyo yasihi kufanya uadilifu, hisani na kutoa haki wanavyotolewa jamaa wa karibu kwa kila daraja, yanakatalia mbali dhuluma na uasi. Islam inasema, fanyeni uadilifu. Kati ya kuyatekeleza sana mno mafundisho haya ya Kurani tunaona mfano bora ndani ya maisha ya Mtume Mtukufu s.a.w. Mtu ambaye si Mwislamu, bali ni Myahudi, anapomjia ili kupata adili na anamshitaki Mwislamu, Mtume Mtukufu s.a.w., baada ya kusikiliza pande zote mbili akatoa uamuzi kwa Myahudi dhidi ya Mwislamu[14] Siku hizi tunaona mtu binafsi au serikali zinachukua mkopo, lakini wakati wa kulipa wanatafuta udhuru kadhaa. Mfano wa Mtume Mtukufu s.a.w. tunaona — na mfano wake ndio mafundisho ya kweli ya Kiislamu — ni huu kwamba si tu alikuwa akimrudishia mkopeshaji deni akidaiwa kabla ya wakati uliopangwa, bali akifanya hisani alikuwa akitoa zaidi kiasi fulani. Naam, nilikuwa naongea kuhusu vita, basi kuhusu wafungwa wa vita Mwenyezi Mungu Anasema:

---

[14] Musnad Ahmad bin Hambal, J. 5 uk. 336, Musnad Ibn Abi Hadrad Hadith Na. 15570, ‘Alamul-Kutub, Beirut 1998.

مَا كَانَ لِنَبِيٍّ اَنۡ يَّكُوۡنَ لَهٗۤ اَسۡرٰى حَتّٰى يُثۡخِنَ فِى الۡاَرۡضِ ؕ[15]

Haimpasi Nabii kuwa na wafungwa wa vita mpaka apigane vita ya umwagaji damu ardhini.

Katika zama zile ambapo ilikuwa desturi ya kuwafanya watu wa kabila la adui kuwa wafungwa, Islam yapaza sauti kwamba ni kinyume cha uadilifu kumfanya mtu kuwa mfungwa, ambaye haingii katika vita ili kipigana dhidi ya Islam. Kama siku hizi serikali, au serikali za jina wanafanya hivyo kwa jina la Islam, basi hiyo ni kinyume cha mafundisho ya Islam, hiyo haijuzu kabisa. Kisha kuhusu wafungwa hao ambao ni wafungwa wa vita, Islam inasema:[16] فَاِمَّا مَنًّۢا بَعۡدُ وَ اِمَّا فِدَآءً Na wafungwa wa vita watatendewaje? Kasema, ama waacheni waende zao kwa kuwafanyia hisani au kwa kupokea fidia waacheni huru.

Tena wafungwa wa vita watendewa vyema zaidi. Katika vita za zama zile kila mmoja alikuwa na jukumu la kujitayarishia zana za vita, na akitekwa katika vita alitakiwa mwenyewe ajaribu kujipatia uhuru au watu wa familia yake wakafanya mpango. Wakati mwingine katika hali hizo baadhi ya jamaa walikuwa wanapatwa na nia mbaya ya kutwaa mali na kumbakiza aliyetekwa katika

[15] Al-Anfaal, 8:68

[16] Muhammad, 47:5

hali ya kutekwa. Kama hawapo jamaa wa karibu, basi jamaa wa mbali walikuwa wakitenda hivyo. Au pengine sababu nyingine fulani inatokea inayomfanya mfungwa asiweze kutoa fidia, hapo Kurani imesema:

وَالَّذِيْنَ يَبْتَغُوْنَ الْكِتٰبَ مِمَّا مَلَكَتْ اَيْمَانُكُمْ فَكَاتِبُوْهُمْ اِنْ
عَلِمْتُمْ فِيْهِمْ خَيْرًا ۖ وَّاٰتُوْهُمْ مِّنْ مَّالِ اللّٰهِ الَّذِيْٓ اٰتٰىكُمْ ۚ[17]

Yaani, miongoni mwa wafungwa wenu wa vita ambao hamwezi kuwaacha huru kwa kuwafanyia hisani wala kaumu yao haikuwaachisha kwa kutoa fidia zao, kama wakiwaombeni kwamba tuachwe huru tutatoa fidia yetu kwa kupata pesa kwa kufanya kazi na kutumia ufundi wetu, basi waacheni huru mkiona wanaweza kujichumia riziki wakiwa huru; bali chukueni hatua ya mbele ya hisani kwamba wasaidieni katika juhudi yao hiyo. Na Waislamu wakiwa wasaidizi wao, wawasaidie kwa mali yao, na wajaribu kuwaachisha huru kwa kuwasaidia kwa mali.

Wanaopiga kelele siku hizi za kuimarisha uadilifu pia hawawezi kuonyesha kiwango hicho hata hawawezi kukikaribia. Baadhi ya vyama vya haki za kibinadamu vinadai kufanya kazi hiyo, lakini licha ya wafungwa wa vita, hata wafungwa kisiasa na kwa jina la dini pia

---

[17] An-Nuur, 24:34

haviwezi kuwaachisha. Kama nilivyosema hapo kabla pia, Waislamu vilevile wameshasahau mafundisho ya dini. Wakizingatia mafundisho hayo, wanaofungwa bila sababu na Islam inaharibiwa jina, basi hawatafanya hivyo. Kwa vyovyote tunazungumzia mafundisho ya Islam. Basi, Islam inaimarisha haki za uhuru wa mtu kiasi hiki kwamba mtu wa kaumu ya maadui anayeinua upanga dhidi ya Waislamu akiingia vita kwa sababu ya uadui wa Islam, anapofungwa kwa kushindwa vitani au kwa sababu fulani, Islam inasema jaribuni kumwacha huru adui wa aina hii mkifanya hisani. Nilieleza sasa hivi kwamba leo inahalalishwa kuitupia Japan mabomu ya kiatomiki ambayo yaliua idadi kubwa ya wananchi wasio na hatia. Mtu mmoja alikaa kwenye ngazi — mkiziona picha — huyo akabaki pale pale katika hali iyo hiyo na ngozi yake ikiyeyuka ikatundikika na akawa sanamu papo hapo. Tena baada ya waliokufa mara moja, vifo viliendelea kutokea kwa muda mrefu kwa athari ya mnururisho, watoto walemavu wakaendelea kuzaliwa. Leo baada ya muda mrefu kwa kuzungumzia vita ile ya Japan na kuzungumzia bomu la kiatomiki watu hao wanataka nini? Je, kwa jambo hili wanawachochea wanaotaka kudhulumu. Mtume Mtukufu s.a.w. alisema kwamba katika hali ya vita adui anayeshambulia, baada ya kumshinda pia hakuna ruhusa kwa vyovyote kuharibu

sura yake. Hakuna kudanganya kwa njia yoyote hata katika vita.[18] Msimwue mtoto wala mwanamke, msiwaue mapadri na viongozi wengine wa dini. Msiwaue wazee, watoto na wanawake.[19] Daima kumbukeni suluhu na hisani. Mkilazimika kupigana vita na kushambulia nchi fulani, basi msieneze hofu huko wala msitumie nguvu kwa watu wa kawaida.[20] Majeshi yapitie njia zisizowasumbua raia.[21] Msimjeruhi adui usoni. Yapasa kumtia adui hasara kidogo iwezekanavyo.[22] Kama Mwislamu akimdhuru mfungwa wa vita isivyojuzu, basi aachwe huru mara moja, yaani huyo mfungwa.[23] Mwangalie raha ya wafungwa. Kama wapo wafungwa walio jamaa, wasitengwe bali wawekwe pamoja.[24] Mtu

---

[18]Sahih Muslim Kitabul-Jihad was-Siyar, Baabu Ta'miril-Imamil-Umaraa, Hadith Na. 1731.

[19] Musnad Ahmad bin Hambal, J.1, uk. 768, Musnad ʻAbdullah Bin ʻAbbas, Hadith Na. 2728, ʻAlamul-Kutub Beirut 1998.

Sunan Abi Dawud, Kitabul-Jihad, Baabu Fi Duʻail-Mushrikin, Hadith Na. 2614.

[20]Sahih Muslim Kitabul-Jihad was-Siyar, Baabu fil-Amr bit-Taisir wa Tarkit-Tanfir Hadith Na. 1732.

[21] Sunan Abi Dawud, Kitabul-Jihad, Baabu ma yuʻmaru min indhimamil-ʻAskar wa Saʻatihi Hadith Na. 2629.

[22] Sahih Bukhari Kitabul-ʻItq baabu Idha Dharabal-ʻAbda Falyajtanibil-Wajha Hadith Na. 2559.

[23] Sahih Muslim, Kitabul-Iman wan-Nudhur Baabu Suhbatil-Mamalik wa Kaffaratil-Liman latama ʻAbdahu, Hadith Na. 1659.

[24] Sunan At-Thirmidhi Abwabus-Siyar, Baabu fi Karahiyatil Tafrik Bainas-Sabyi, Hadith Na. 1566.

aliye na mfungwa, amlishe anachokula yeye mwenyewe. Mambo hayo yote ni nini? Hayo yameuacha uadilifu nyuma kabisa, hayo yote ni hisani. Yu nani anayewatendea hivyo wafungwa wa vita?

Basi, hakuna fundisho lolote la zamani linaloweza kukabiliana na mafundisho hayo wala kanuni za wadai wa siku hizi wa haki za wanadamu haziwezi kuukabili uadilifu huo na hisani hiyo ya kiwango cha juu. Mambo hayo niliyoyaeleza kwamba mtawatendea wafungwa sio kwa kuendeleza vita bali ni kwa kukomesha vita. Mtume Mtukufu s.a.w. alipofanya Mkataba wa Madina, akawapa Wayahudi wa Madina haki zile zile walizokuwa nazo Waislamu kwamba hawatadhulumiwa na waaminio, na kama wakidhulumiwa na waaminio au na wengine wowote, basi watasaidiwa dhidi ya dhuluma hiyo.[25] Kipengele hiki kati ya vipengele vingi vya Mkataba kinawatolea Wayahudi dhamana ya amani kwamba wakipenda wakae katika Madina au wakitaka waondoke. Huo ndio uadilifu alioimarisha Mtume Mtukufu s.a.w. Kama Waislamu wajipatie kiwango hiki na washikamane na mikataba yao, kamwe hawatapata dhila. Historia ya Waislamu inaeleza kwamba maadamu waliendelea

---

[25]As-Siratun-Nabawiyyah Libni Hisham, uk. 354-355, Hijratur-Rusul[saw] Darul Kutubil-'Ilmiyyah, Beirut 2001.

kushikamana na mapatano yao, waliendelea kupata maendeleo. Walipoacha tu kushikamana na ahadi zao na kutengana na uadilifu, papo hapo dhila yao ikaanza. Anagalieni, ni mfano bora wa hali ya juu namna gani wa kutimiliza ahadi kwamba wakati jeshi la Kiislamu lilipoanza kurudi nyuma kwa sababu ya mashambulio ya Warumi, hapo Waislamu waliwarudishia wasiokuwa Waislamu kodi yao wakisema kwamba tulichukua kodi hii kwa kuwalindeni na kuimarisha amani katika eneo hili, lakini hatukuweza, kwa hiyo sasa hatuna haki ya kuchukua kodi. Jibu walilotoa watu wa sehemu hiyo pia ni tukio la ajabu katika historia ya dunia, linapaswa kuitwa tukio la muhimu sana lifaalo kutukuzwa. Wakasema, tulikuwa tunadhulumiwa na watu wa dini yetu sisi wenyewe, mkaja hapa, mkashika utawala, na kwa kushikamana na ahadi yenu kwa viwango vya juu sana vya uadilifu wenu mkatuvutia. Sasa tukiungana nanyi tutapigana vita. Basi Waislamu waliwashinda jeshi la Rumi na wakaimarisha utawala wao. Na Waislamu walipoingia mjini, wakazi wa hapo waliwapokea kwa jazba sana.[26] Laiti serekali za Waislamu za siku hizi pia zipate somo na zikome kuwadhulumu watu wao na wengine, basi dhila na fedheha zao zitageuka kwa sababu

---

[26]Kitabul-Kharaj na Qadhi Abu Yusuf, uk. 149-151, Faslun fil-Kanaisi wal-Biya'i was-Sulban.

ya wao kuwa viongozi wa dunia. Lakini kwa ajili yake watalazimika kuitikia sauti ya Mwenyezi Mungu anayotufikishia Imamu wa zama. Mada hii ya uadilifu, hisani na utoaji kwa jamaa wa Karibu[27] imetajwa mara nyingi sana katika Kurani Tukufu. Maisha ya Mtume Mtukufu s.a.w. nayo yamejaa habari hii. Tena katika zama hizi tunakuta mada hii katika sehemu nyingi za maandishi ya Hadhrat Masihi Mau'udi a.s. ambayo yakielezwa, masaa yatahitajika — yaani aliyoeleza moja kwa moja katika maelezo ya aya hiyo. Wakati huu nitataja jambo moja jingine linalodhihirisha jazba ya Mtume Mtukufu s.a.w. ya kuwatolea jamaa wa karibu kwa ajili ya wanadamu waliopotea — sio kwa waaminio, bali kwa wanadamu, kwa washirikina pia, kwa makafiri pia na kwa dini zingine pia, Alilohifadhi Mwenyezi Mungu katika Kurani Tukufu. Alihuzunika kwa waliotengana na Mwenyezi Mungu, na huzuni zenyewe hizo zilikuwa kwa sababu tu kwamba kwa kutengana na Mungu wanajiharibia akhera yao na kujipatia ghadhabu ya Mwenyezi Mungu, na hivyo watastahiki kupata adhabu ya Mwenyezi Mungu. Jazba ya kuwahurumia watu aliyokuwa nayo moyoni mwake ilikuwa nyingi zaidi kuliko hata ile ya mama na baba. Jazba ile ilimfanya

---

[27] An-Nahl, 16:91

asipate utulivu usiku wala mchana, kana kwamba alijitia katika mahilikisho kwa kuwasumbukia. Kwa kuona mahangaiko hayo na kiherehere hicho Mwenyezi Mungu Alimwambia:

لَعَلَّكَ بَاخِعٌ نَّفۡسَكَ اَلَّا یَکُوۡنُوۡا مُؤۡمِنِیۡنَ ○[28]

Je, utajihilikisha kwani hawaamini? Hisia kwa wanadamu wote kuwa jamaa wa karibu haziwezi kudhihirika kuzidi hizo. Si kwa kuongeza idadi ya wafuasi wake, bali hisia hizo zilikuwa kwa sababu ya kuudhika kwa ajili yao. Kisha wapingaji wanaleta shutuma kwamba makundi ya Islam yenye siasa kali wanafanya matendo hayo kwa sababu ya mafundisho ya Islam au Mungu apishe mbali, Mtume Mtukufu s.a.w. mwenyewe analaumiwa. Wanatenda hivyo kwa sababu ya kuachana na mafundisho sahihi ya Islam. Basi, kama nilivyosema, kwa kufuata Islam ya kweli Waislamu hawana haja ya kundi lenye siasa kali, bali wanamhitaji Mjumbe wa Mwenyezi Mungu. Na wapingaji wa Islam pia wafumbue macho yao na watumie akili na watazame mafundisho mazuri ya Islam. Leo ni jukumu la kila Mwahmadiyya kwamba atekelezapo agizo la uadilifu, hisani na kuwatolea jamaa wa karibu kwa kila jiha ya maisha yake, amfikishie pia ujumbe huu kila mtu

---

[28] Ash-Shu'araa, 26:4

wa dunia. Awaambie, sikilizeni sauti ya Mjumbe wa Mungu wa zama hizi. Tambueni uchungu wake aliokuwa nao moyoni mwake kwa kumfuata Bwana wake ambaye Mwenyezi Mungu pia alimwambia kwamba utajihilikisha.

لَعَلَّكَ بَاخِعٌ نَّفۡسَكَ اَلَّا يَكُوۡنُوۡا مُؤۡمِنِيۡنَ ۝[29]

Mwenyezi Mungu Atujaalie sote tuwe na uchungu huo kwa ubinadamu. Inapaswa pia kujaribu kuuzalisha huo uchungu sawa na hisia na hali ya kila moja na sawa na kiwango kilivyo. Na dunia badala ya kwenda kwa maangamio ijisalimishe ikielewa somo la uadilifu, hisani an kuwatolea jamaa wa karibu. Na Mwenyezi Mungu Aijaalie dunia kuielewa hiyo na kuifanya dunia hii kuwa Pepo na Mwenyezi Mungu Aiandalie dunia sababu za kupata Pepo ya akhera pia.

Sasa tutafanya maombi. Ni fadhili kubwa na hisani ya Mwenyezi Mungu kwamba Ameubariki mkutano huu kwa namna zote, kimahudhurio pia, na kwa hali ya hewa pia. Mwenyezi Mungu Awapelekeni nyote kwenu kwa usalama. (Maombi) Assalamu Alikum. Watu ambao wamekaa mbele yangu katika sehemu ya rangi ya kijani waendelee kukaa, hawana ruhusa ya kusimama, walio jukuaani nao waendelee kukaa.

---

[29] Ash-Shu'araa, 26:4